*Kioo cha Lugha, Juz. 23(1), 1-15*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i1.1

# Uchunguzi wa Mbinu na Vifaa vya Kufundishia Utamaduni wa Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi

*Anitha Nduwamahoro,*[1] *Fiacre Irankeje*[2] *na Dieudonné Butoyi*[3]

## Ikisiri

Makala hii imelenga kuchunguza mbinu na vifaa mbalimbali vinavyotumiwa na walimu kufundishia utamaduni wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi. Katika ukusanyaji wa data, hojaji na ushuhudiaji ndizo mbinu zilizotumiwa. Nadharia ya Utamaduni-Jamii ya Vygostsky (1980) ilitumika katika uchanganuzi wa data. Data ilichambuliwa kwa kutumia majedwali, maelezo na programu tumizi ya kuchambua data ya SPSS *(Statistical Package for the Social Sciences).* Matokeo yameonesha kuwa baadhi ya walimu wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi wanaingiza masuala ya utamaduni katika ufundishaji na wanatumia mbinu tano katika ufundishaji wao. Hata hivyo, matokeo yameonesha kwamba mbinu mbili ambazo ni uigizaji na majadiliano kuhusu vitabu na matini za Kiswahili ndizo zinazotumiwa kwa kiwango kikubwa. Kuhusu vifaa vya kufundishia masuala ya utamaduni wa Kiswahili, utafiti huu umedhihirisha kuwa vitabu, intaneti, projekta na kompyuta ndivyo vifaa vinavyotumiwa kwa asilimia kubwa. Walimu wameshauriwa kubuni mbinu na vifaa vinavyoweza kuwasaidia kufanikisha mafunzo ya utamaduni wa Kiswahili kwa sababu lugha na utamaduni havitenganishwi.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazofundishwa katika idara mbalimbali za vyuo vikuu nchini Burundi. Mtu yeyote anayejifunza lugha ya kigeni analenga kupata umilisi wa kiisimu wa lugha hiyo ili kuitumia kwa ufasaha katika mawasiliano (Macaro, 2003). Hata hivyo, ujifunzaji wa lugha haulengi tu kumudu kanuni za kiisimu bali pia kupata umilisi wa kiutamaduni ili mjifunzaji aitumie kwa

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kirundi-Kiswahili, Chuo Kikuu cha Burundi.
Baruapepe: nduwanith@gmail.com

[2] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kirundi-Kiswahili, Chuo Kikuu cha Ualimu (ENS-Burundi).
Baruapepe: irankejefiacre@gmail.com

[3] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha na Tamaduni za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Burundi.
Baruapepe: dbutoyi17@gmail.com

kuzingatia muktadha na utamaduni wa lugha hiyo (Macaro, 2003). Hivyo, lugha na utamaduni huwa na uhusiano usio wa kifani na hutegemeana. Lugha huchukuliwa kama chombo cha kuelezea na kuendeleza utamaduni wa jamii yoyote (Matinde, 2012). Hivyo basi, uhusiano uliopo kati ya lugha na utamaduni ni imara kwa sababu lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii fulani na pia ni njia ya kusambaza maadili ya tamaduni, kanuni na imani za jamii.

Lugha ndiyo inayoonesha sura ya jamii. Uhusiano huo unadhihirisha kwamba kujifunza lugha ya kigeni ni kujifunza utamaduni wake pia (Ali, 2017). Mtu ajifunzaye lugha bila kuzingatia utamaduni wa lugha husika huweza kuiharibu. Jambo hilo linamaanisha kwamba, mwanafunzi wa lugha ya kigeni hawezi kuwa mahiri wa mawasiliano baina ya lugha za tamaduni tofauti wakati hazingatii utamaduni wa lugha hizo (Bennet na Allen, 2003).

Hivyo, lugha haichimbuki katika hali ya upweke, bali ni zao la utamaduni fulani (Ali na Mahar, 2015; Ali, 2017). Ili kufanikisha mchakato wa ujifunzaji wa lugha za kigeni, wanafunzi na walimu hawapaswi kuzingatia maarifa yahusianayo na sarufi ya lugha tu na kupuuza utamaduni wa lugha husika kwa sababu utamaduni na lugha ni kama pande mbili za sarafu moja (Ali na Mahar, 2015; Emitt na Komesaroff, 2003). Vilevile, utamaduni huathiri ufundishaji wa lugha kiisimu na kielimu. Kiisimu, viwango vya semantiki, pragmatiki na stadi za mazungumzo huathiriwa. Kielimu, utamaduni unashawishi uteuzi wa vifaa vya kufundishia kwa sababu utamaduni wa lugha unaopatikana katika masomo pamoja na msingi wa kiutamaduni upatikanao katika mbinu za ufundishaji unapaswa kuzingatiwa wakati wa kuamua vifaa vya kutumika kufundishia lugha (McKay, 2003).

Kutokana na ufafanuzi hapo juu, ni dhahiri kwamba kufundisha utamaduni wa wanajamiilugha fulani ni suala ambalo haliwezi kupingwa kwa sababu ni muhimu kwa maendeleo ya lugha na ujuzi wa kuwasiliana baina ya tamaduni tofauti. Ni dhahiri kwamba, lengo kuu la ujifunzaji wa lugha ya kigeni ni kuweza kuwasiliana na wenyeji pamoja na watumiaji wa lugha husika. Kwa hiyo, ili mwanafunzi aweze kuwasiliana vilivyo na wenyeji pamoja na watumiaji wa lugha ya kigeni anayojifunza, ni lazima afundishwe utamaduni mpya wa wanajamiilugha lengwa. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Burundi pamoja na wahitimu wanashindwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa namna inayowiana na utamaduni wa Kiswahili katika mawasiliano yao (Bamporubusa, 2012; Nduwamahoro, 2021; Ndayisenga, 2022; Butoyi, 2022). Hivyo, kwa kuwa Kiswahili kimekuwa kikifundishwa kama lugha ya kigeni katika Chuo Kikuu cha Burundi tangu mwaka 1978 (Bukuru na Niyonkuru, 2016; CRELACS, 2023; Muaka, Nduwamahoro na Butoyi, 2024), ni muhimu kuchunguza ikiwa suala la utamaduni wa Kiswahili linatiliwa mkazo katika ufundishaji wa lugha hiyo. Kwa mantiki hiyo, programu yoyote ya ufundishaji inapoandaliwa na kuanza kutekelezwa, inatakiwa kutathminiwa ili kuchunguza ufanisi na udhaifu wake na kuboresha sera za mpangilio wa masomo (UNODC,

2017; Nduwamahoro, 2021). Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuchunguza mbinu zinazotumiwa katika kufundisha vipengele vya utamaduni wa Kiswahili katika Idara ya Lugha na Tamaduni za Kiafrika na Idara ya Kirundi-Kiswahili za Chuo Kikuu cha Burundi. Pia, umechambua vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wake. Uteuzi wa idara hizo umetokana na kwamba ndizo idara zinazohusika na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama kozi muhimu na ya lazima. Vilevile, Kiswahili kinatumiwa kufundishia baadhi ya kozi katika idara hizo.

## 2.0 Mapitio ya Kazi Tangulizi na Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

Sehemu hii imeshughulikia maandiko mbalimbali yanayohusu ufundishaji wa utamaduni katika ujifunzaji wa lugha za kigeni na ufafanuzi wa dhana muhimu katika utafiti huu.

### 2.1 Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

Katika sehemu hii dhana muhimu zilizotumika katika makala hii zimefafanuliwa. Ili kuielewa vizuri makala hii,ni muhimu kuzielewa dhana hizo. Aidha, dhana hizo zimefafanuliwa kulingana na maandiko yaliyoshughulikiwa katika makala hii. Dhana hizo ni utamaduni na lugha.

#### 2.1.1 Dhana ya Utamaduni

Utamaduni ni jumla ya shughuli, kumbukumbu, matumaini, mipango ya baadaye ya jamii fulani pamoja na ndoto na maono yao (Liyong, 1972). Vilevile, utamaduni ni jumla ya mfumo wa asasi, amali, mielekeo, fikra na desturi zinazoitambulisha jamii fulani katika kipindi fulani cha historia (King’ei na Kobia, 2007). Mfumo wa imani na fikra unaotokana na utaratibu wa elimu, mafunzo na mila au desturi na ambao unawezesha kukomaa kwa watu wa jamii fulani pia unaitwa utamaduni (King’ei na Kobia, 2007). Hivyo basi, utamaduni hujumuisha vipengele vingi kama vile lugha, maadili ya kijamii, imani, fikra, mila na desturi.

#### 2.1.2 Dhana ya Lugha

Lugha ni mfumo wa ishara ambazo kwazo watu wanawasiliana (Todd, 1987). Pia, ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana (TUKI, 1990). Hivyo, lugha ni chombo cha mawasiliano ambacho huwawezesha watumiaji wake kupashana ujumbe na hisia (Yule, 1983; Shreeb, 2009, Masebo na Nyangwine, 2016; Butoyi, 2022). Vilevile, lugha ni mojawapo ya vipengele vya utamaduni ambavyo watu katika jamii hutumia katika kubadilishana mawazo. Kupitia lugha, watu katika jamii wanaweza kuelezea maadili yao ya kitamaduni, imani, kanuni za jamii, na mengineyo (Shreeb, 2009; Zou, 2012). Hivyo, lugha ni kitambulisho cha mtu katika jamii ya watu wengi wenye tamaduni tofauti. Pia, lugha ni chombo muhimu ambacho wanajamii hutumia katika uwasilishaji wa ujumbe, maarifa/ujuzi, maswali

yanayoikumba jamii na maadili kwa kila mmoja na kuyapitisha kwa kizazi kijacho.

### 2.2. Ufundishaji wa Utamaduni katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni

Gao (2006) katika utafiti wake alieleza kwamba ufundishaji wa utamaduni ni ufundishaji wa lugha. Kwa mujibu wa utafiti wake, walimu wanaofundisha lugha ya kigeni lazima watambue mazingira ya kufundisha utamaduni katika darasa la lugha na wajaribu kuongeza utambuzi kwa wanafunzi juu ya utamaduni na kuboresha ujuzi wao wa kuwasiliana. Wang na Kulich (2014) wanadai kwamba ufundishaji wa lugha ya kigeni unaambatana zaidi na utamaduni wa lugha husika. Kwa mantiki hiyo, ufundishaji wa lugha ya kigeni unapaswa kuambatana na ufundishaji wa masuala ya kitamaduni ya lugha husika ili wanafunzi wa lugha hiyo waimarike katika mawasiliano na wenyeji wa lugha husika.

Cakir (2000) anadai kuwa lugha hufundishwa na kutumiwa katika muktadha unaotawaliwa na utamaduni na shughuli tofauti ambazo lazima ziimarishwe na wanafunzi wa lugha ikiwa wataidhibiti lugha kama wasemaji asilia wanavyoidhibiti. Hivyo, wanafunzi wa lugha ya pili wanapaswa kufunuliwa katika mazingira mbalimbali ya kitamaduni ambapo wanaweza kujifunza lugha kwa vitendo. Naye Stern (1992) anafafanua mambo ya kitamaduni ya kufundishwa katika ujifunzaji wa lugha ya kigeni kuwa yanahusisha maeneo, namna ya kipekee ya kujiandaa kimaisha, watu na jamii kwa ujumla, historia, taasisi na sanaa, muziki na fasihi. Mtafiti huyo amesema kuwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni, namna ya kipekee ya kuandaa maisha ni kipengele muhimu zaidi ambacho walimu na wanafunzi wanahitaji kuzingatia kama mada ya kitamaduni ya kutilia mkazo. Sababu ni kuwa hili hujumuisha mambo ambayo mtu binafsi anatakiwa kutambua, kuelezea, kutenda, kula, kupenda, kutopenda, kuvumilia, na kuhifadhi kwa njia inayofaa na inayowezekana katika hali tofauti ya maisha.

Zaidi ya hayo, Kumaravadivelu (2008) na Moore (2003) wanaonesha kwamba wanafunzi wa lugha za kigeni wanahitaji kufundishwa masuala ya kitamaduni ya matumizi ya lugha. Aidha, wanakiri kuwa mambo hayo ya kitamaduni yanachochea hamu ya mwanafunzi katika ujifunzaji wa lugha hiyo na kuwashirikisha kihisia katika matumizi ya lugha ya kigeni na mawasiliano kwani jambo hilo hulenga shughuli zao za maisha ya kila siku. Vilevile, Belkhir-Benmostefa (2017) anabainisha nyenzo za kufundishia masuala ya utamaduni kwa wageni kama vile vitabu, majarida na magazeti, mashairi na habari ndogondogo, intaneti na rekodi na kudhihirisha kuwa huwa walimu hawatumii nyenzo hizo, jambo ambalo linakwamisha ujifunzaji wa utamaduni kwa wanafunzi.

Msigwa (2019) alichunguza mchango wa media za video katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Utafiti huu ulifanyika kwenye kituo cha MS TCDC1 (MS Training Center for Development Cooperation) na matokeo yanabainisha kuwa ufundishaji wa Kiswahili kwa video ni muhimu kwa kuwa huwasukuma

wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kupenda kujifunza lugha hiyo. Vilevile, imethibitishwa kuwa video huwapa hamasa wanafunzi katika kujifunza lugha.

Nao Vicent na Msigwa (2021) walichunguza umuhimu na changamoto za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Matokeo yalionesha kuwa kuna umuhimu wa kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni kwani, TEHAMA inaufanya ufundishaji uwe rahisi na kuokoa muda kwa kufundisha mambo mengi katika muda kidogo, na kumpunguzia mwanafunzi uchovu na gharama. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yamebaini changamoto kadhaa za matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni, kama vile ukosefu wa vifaa vya kutosha, uhaba wa miundombinu na ujuzi duni wa walimu katika matumizi ya TEHAMA.

Mwisho, Ali (2017) alitafiti kuhusu utoaji wa maelezo ya utamaduni katika kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni. Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa walimu wanatumia mbinu mbalimbali kutoa maelezo ya utamadunikama vile kuonesha vitendo vya kiutamaduni, kutoa maelezo yaliyobainishwa katika vitabu na kulinganisha na utamaduni. Hata hivyo, utafiti wake ulithibitisha kuwa mbinu zinazotumika haziwasaidii sana walimu kufundisha wanafunzi wa kiwango cha awali kwa urahisi zaidi.

Kutokana na maandiko hayo hapo juu, ni dhahiri kwamba suala la ufundishaji na ujifunzaji wa vipengele vya utamaduni wa lugha kwa wageni limewashughulisha watafiti mbalimbali. Maandiko hayo yanaonesha mbinu na nyenzo za kutumia katika utoaji wa maelezo ya utamaduni wa lugha na kuthibitisha kuwa ufundishaji wa lugha hautenganishwi na ufundishaji wa utamaduni. Hivyo, ni lazima wanafunzi wafundishwe masuala ya utamaduni wa lugha wanayojifunza ili kuweza kufanikisha mawasiliano. Hata hivyo, baadhi ya tafiti zimedhihirisha kwamba walimu hawatumii nyenzo hizo na huteua mbinu zisizowasaidia kufanikisha ufundishaji wa utamaduni wa lugha kwa wanafunzi. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza mbinu na vifaa vinavyotumiwa kufundishia utamaduni wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi. Tofauti na tafiti hizo tangulizi, utafiti huu umechunguza kwanza ikiwa masuala ya utamaduni wa Kiswahili yanajadiliwa darasani na kubainisha mbinu na nyenzo zinazotumiwa na walimu kuyasambaza kwa wanafunzi wa Burundi.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utamaduni-Jamii iliyoasisiwa na Vygostsky (1980). Chanzo cha kuibuka kwa nadharia hii ni kwamba nadharia zilizotangulia hazikuzungumzia masuala ya uzingativu wa utamaduni katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili au ya kigeni (Vygostsky, 1980; Ali, 2017). Kwa mujibu wa nadharia hii, lugha hutambulika kama stadi inayoendelezwa katika muktadha wa kiutamaduni-jamii. Hivyo, jamii ina athari kubwa kwa mwanafunzi katika kufungamana na utamaduni wa lugha anayojifunza

na kupata umilisi wa lugha ya jamii husika (Lantolf, 1994; Ali, 2017). Kwa hiyo, ili mwanafunzi afikie kiwango cha juu cha umilisi wa lugha anayojifunza, hana budi kuwa mjuzi wa stadi ya utamaduni wa lugha hiyo.

Nadharia hii imetumiwa katika utafiti huu kwa kujikita kwenye mihimili yake kama ilivyoelezwa na Ali (2017). Mihimili hiyo ni, kwanza, upatanisho ambao unadai kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili lazima uhusishe masuala ya utamaduni wa lugha hiyo. Mhimili huu umetumiwa na watafiti katika kubainisha ikiwa masuala ya utamaduni wa Kiswahili yanajadiliwa kwenye Chuo Kikuu cha Burundi. Mhimili wa pili ni uingizaji ubongoni ambao ni uhusianishaji wa ishara na shughuli mbalimbali za kisaikolojia. Kwa kujikita kwenye mhimili huu, watafiti wamebainisha vifaa na mbinu muhimu zinazotumiwa kusaidia wanafunzi kumudu masuala ya utamaduni. Mhimili wa tatu ni tafakuri ambayo ni hali ya kutumia akili kwa kuhusisha na jamii hasa katika kung'amua changamoto mbalimbali katika kuelewa mambo. Hivyo, changamoto za kisaikolojia zinaonesha jinsi mtu anavyoweza kuhimili namna ya kufundisha mambo mbalimbali kutoka katika jamii au aina fulani ya maisha. Mhimili huu umezingatiwa katika kutoa maelezo juu ya namna mbinu na vifaa bainifu vinavyotumiwa na walimu ili kuwafundisha wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Burundi masuala ya utamaduni. Hivyo basi, nadharia hii imeuongoza utafiti huu katika kuchunguza na kuchanganua mbinu na vifaa halisi vinavyotumiwa wakati wa ufundishaji wa utamaduni wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi.

## 4.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Chuo Kikuu cha Burundi. Watoataarifa walipatikana kutoka Idara za Kirundi-Kiswahili na Lugha na Tamaduni za Kiafrika. Sababu ya uteuzi wa idara hizo ni kuwa, katika idara hizo, Kiswahili ni kozi muhimu na ya lazima na pia lugha mojawapo miongoni mwa lugha za kufundishia. Katika utafiti huu, sampuli ilihusisha walimu 8 ambao ndio walimu wa Kiswahili kutoka katika idara hizo. Hawa walichaguliwa kwa usampulishaji lengwa ambao uliwakusudia walimu wanaofundisha Kiswahili katika idara hizo. Usampulishaji lengwa ulitumiwa kwa sababu uliwahakikishia watafiti kuwapata watoataarifa watakaotoa data zenye kuaminika. Katika kukusanya data, hojaji na ushuhudiaji ndizo mbinu zilizotumiwa. Kuhusu mbinu ya hojaji, watafiti waliwakuta kazini watoataarifa na kuwapa hojaji ili wajaze halafu wawarudishie. Watoataarifa walitakiwa kujieleza kwa uhuru ili kupata maoni na mtazamo wao kuhusu mbinu na vifaa wanavyotumia katika ufundishaji wa vipengele vya utamaduni wa Kiswahili. Hojaji ndiyo mbinu kuu iliyotawala ukusanyaji wa data za utafiti huu. Ushuhudiaji ambao ulitumika kama mbinu jazilizi katika utafiti huu, watafiti waliingia katika madarasa ya mwaka wa kwanza, wa pili na wa tatu. Wanafunzi hao ni wale wa idara teule katika kozi za fasihi ya Kiswahili. Watafiti walipata ridhaa ya mwalimu

ili kushuhudia ikiwa masuala ya utamaduni hugusiwa na kuchunguza mbinu na vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji wake.

Mkabala wa kitaamuli ndio uliotumiwa katika uchanganuzi wa data. Mkabala huu uliwaruhusu watafiti kutoa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa ili kuchambua ikiwa malengo yametimizwa. Majedwali na maelezo vimetumiwa katika ufafanuzi wa data. Pia, maswali yamechanganuliwa kwa kutumia programu tumizi ya uchanganuzi wa data (SPSS).

## 5.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Kama ilivyokwishaelezwa katika sehemu ya utangulizi, utafiti huu umelenga kubainisha na kuchunguza mbinu na vifaa vya kufundishia utamaduni wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi. Data kutoka kwa watoataarifa 8 ambao ni walimu zimewasilishwa na kuchambuliwa ili kubainisha mbinu na vifaa wanavyovitumia katika kufundishia utamaduni wa Kiswahili. Hivyo, uchunguzi ulifanyika kwanza ili kubaini kama walimu wana uzoefu katika kufundisha utamaduni wa lugha hiyo. Pia, masuala ya utamaduni yalibainishwa ili kuonesha jinsi yanavyofundishwa kwa wanafunzi wao na kubaini mbinu na vifaa vinavyotumiwa na walimu hao katika ufundishaji.

### 5.1 Uzoefu wa Walimu katika Kufundisha Utamaduni wa Kiswahili

Sehemu hii inajadili matokeo juu ya uzoefu wa walimu wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Burundi katika kufundisha masuala ya utamaduni wa Kiswahili kwa wanafunzi. Jedwali Na. 5.1 linaonesha uzoefu wa walimu katika ufundishaji wa kozi za utamaduni.

**Jedwali Na. 5.1: Uzoefu wa Walimu katika Kufundisha Masuala ya Utamaduni wa Kiswahili**

| Na. | Idadi ya Walimu | Miaka ya Uzoefu |
|---|---|---|
| 1. | 1 | 30 |
| 2. | 1 | 4 |
| 3. | 1 | 1 |
| 4. | 5 | 0 |

**Chanzo:** Uwandani (2023)

Jedwali Na. 5.1 linaonesha kwamba walimu watatu tu ndio walio na uzoefu wa kufundisha utamaduni wa lugha ya Kiswahili. Mmoja ana uzoefu wa miaka 30, mmoja miaka 4 na mwingine mwaka 1. Wengine watano walithibitika kuwa hawana uzoefu katika kufundisha utamaduni wa Kiswahili. Maelezo ya watoataarifa yalidhihirisha kwamba walimu watano wanafundisha kozi za isimu ya Kiswahili na stadi za lugha na kuwa hawagusii masuala ya utamaduni wa Kiswahili darasani. Matokeo hayo yanaonesha kuwa walimu wengi wa Kiswahili

katika Chuo Kikuu cha Burundi, yaani watano kati ya wanane wanaofundisha Kiswahili, hawana uzoefu wa kufundisha masuala ya utamaduni wa lugha hiyo.

### 5.2 Maoni ya Walimu kuhusu Umuhimu wa Uingizaji wa Masuala ya Utamaduni katika Ufundishaji wa Kiswahili

Programu za ufundishaji wa Kiswahili za vyuo vikuu nchini Burundi haziyapi kipaumbele masuala ya utamaduni. Hivyo, hakuna kozi inayolenga kufundisha utamaduni wa lugha ya Kiswahili (Nduwamahoro, 2021). Hii ina maana kuwa mtaala unajikita kwa kiasi kikubwa kwenye masomo ya sarufi. Walimu wanaofundisha masuala ya utamaduni huyaweka kwenye utashi wao. Hivyo, katika sehemu hii, watafiti wamechunguza ni walimu wangapi wanaona umuhimu wa uingizaji wa masuala ya utamaduni wa lugha ya Kiswahili katika ufundishaji wa baadhi ya masomo, angalau katika yale yanayohusu fasihi ya Kiswahili. Jedwali Na. 5.2 linaonesha idadi ya walimu wanaoona kuwa ni muhimu kuingiza masuala ya utamaduni katika darasa la Kiswahili.

**Jedwali Na. 5.2: Umuhimu wa Uingizaji wa Masuala ya Utamaduni katika Masomo ya Kiswahili**

| **Je, ni muhimu kuingiza masuala ya utamaduni katika ufundishaji wa Kiswahili?** | | **Idadi** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|
| Majibu yaliyotolewa | Ndiyo | 3 | 37.5 |
| | Hapana | 5 | 62.5 |
| | **Jumla ya Majibu** | 8 | 100 |

**Chanzo:** Uwandani (2022-2023)

Matokeo katika Jedwali Na. 5.2 yanaonesha kuwa walimu watatu (37.5%) kati ya wanane waliojaza hojaji, ndio walioona kuwa ni muhimu kuingiza masuala ya utamaduni katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Wengine watano ambao ni sawa na 62.5% walieleza kwamba hawaingizi masuala ya utamaduni wa Kiswahili katika ufundishaji wa lugha hiyo na hawaoni umuhimu wake. Watoataarifa ambao walithibitisha kuwa ni muhimu kuingiza masuala ya utamaduni katika ufundishaji wa masomo ya Kiswahili, walitoa sababu mbalimbali. Kwanza, lugha ni utamaduni na utamaduni hautengani na lugha. Hivyo, usomaji wa matini zinazohusu nyanja tofauti za utamaduni wa Kiswahili huwasaidia wanafunzi kuelewa misingi ya lugha ya Kiswahili. Pili, msamiati mpya ukielezwa kwa mifano itokayo katika utamaduni wa Kiswahili, inasaidia kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi. Tatu, walimu wanaona kuwa kudokeza filamu

fupifupi zinazohusu utamaduni wa Waswahili husaidia wanafunzi kukariri masomo ya darasani na kuamsha mapenzi yao kwa lugha ya Kiswahili. Maoni hayo yanashadidiwa na Msigwa (2019) ambaye anaonesha kwamba wanafunzi wanapofundishwa kwa mfano na kutazama video zinazoonesha matumizi ya Kiswahili, wanaonjeshwa ladha ya moja kwa moja ya utamaduni wa Kiswahili. Hivyo basi, walimu wanapoleta video au sinema katika darasa, na kuonesha matukio mbalimbali ya jamii kwa wanafunzi, kwa kiasi kikubwa wajifunzaji hupata uelewa mkubwa wa utamaduni wa jamii kupitia matukio hayo.

### 5.3 Masuala ya Utamaduni wa Kiswahili Yanayofundishwa na Walimu

Watoataarifa ambao ni walimu wa masomo ya Kiswahili katika vyuo vikuu waliombwa kuchagua miongoni mwa masuala yaliyoteuliwa na watafiti ambayo huwa yanafundishwa darasani. Jedwali Na. 5.3 hapa chini linaonesha vipengele vya utamaduni vinavyoingizwa katika masomo ya Kiswahili na idadi ya vile ambavyo vilichaguliwa na walimu.

**Jedwali Na. 5.3: Vipengele vya Utamaduni wa Kiswahili Vinavyofundishwa na Walimu**

| **Na.** | **Vipengele vya Kitamaduni** | **Idadi ya Walimu** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mawasiliano kwa mazungumzo | 3 | 37.5 |
| 2. | Shughuli za kijamii | 2 | 25 |
| 3. | Usafiri | 1 | 12.5 |
| 4. | Mavazi na mawasiliano kwa ishara | 1 | 12.5 |
| 5. | Sherehe | 1 | 12.5 |
| 6. | Vyakula na mapishi | 1 | 12.5 |
| 7. | Burudani | 1 | 12.5 |
| 8. | Alama za vitambulisho vya taifa | 1 | 12.5 |
| 9. | Mambo ya kisiasa | 1 | 12.5 |

**Chanzo:** Uwandani (2022-2023)

Matokeo katika Jedwali Na. 5.3 yanaonesha kuwa kipengele cha “mawasiliano kwa mazungumzo” ndicho kinachopewa kipaumbele kikifuatwa na kipengele cha “shughuli za kijamii”. Hivyo, walimu watatu kati ya wanane ambao ni sawa na 37.5%, ndio waliothibitisha kufundisha kipengele cha mawasiliano kwa mazungumuzo. Walimu wawili ambao ni sawa na 25% walisisitiza kuwa kipengele cha “shughuli za kijamii” ndicho muhimu. Vipengele vingine vilivyobainishwa na watoataarifa ni sawa na usafiri, mavazi na mawasiliano kwa ishara, sherehe, vyakula na mapishi, burudani, alama za vitambulisho vya taifa na mambo ya kisiasa. Kila kimoja kilithibitishwa na mwalimu mmojammoja, sawa na 12.5%. Walimu walieleza sababu zao kushadidia kwamba wanafunzi

wakifundishwa vipengele hivyo hapo juu, huwawezesha kupata uelewa na kukomaa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili, kwani lugha ndiyo inayohifadhi utamaduni.

Watoataarifa waliombwa pia kuyataja mambo mengine yanayoendana na utamaduni wa Kiswahili ambayo wanafundisha darasani. Mambo yaliyotajwa ni kama vile vinywaji, nahau na misemo, vitendawili, maamkizi, manunuzi na mahitaji ya kimatibabu, nyimbo, methali, hadithi na mashairi. Mwisho, watafiti walishuhudia baadhi ya masomo ya Kiswahili katika madarasa ya mwaka wa kwanza ya idara za Kiswahili. Somo lililoshuhudiwa linahusu mada ya "Salamu za Kiswahili" na "Nyakati za vitenzi" ambapo mwalimu alitumia mifano kutoka katika maandiko ya kifasihi. Matokeo ya ushuhudiaji yamethibitisha kuwa masuala ya utamaduni wa Kiswahili yanajadiliwa katika baadhi ya masomo ya Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi walielezewa na mwalimu kuwa katika Kiswahili, salamu kwa mtu mkubwa ni "shikamoo", tofauti na Kirundi ambacho salamu huzingatia heshima kuliko rika. Vilevile, mwalimu aliwaelezea kuwa katika utamaduni wa Kiswahili, kuna salamu zinazotolewa tu na watu wa rika moja, kama vile "hujambo?", "hamjambo?" na "hali gani?"

## 5.4 Mbinu Zinazotumiwa na Walimu wa Kiswahili katika Ufundishaji wa Vipengele vya Utamaduni

Mojawapo ya malengo ya utafiti huu ni kubainisha mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa vipengele vya utamaduni vinavyoingizwa katika masomo ya Kiswahili kwenye Chuo Kikuu cha Burundi. Hivyo, watoataarifa walipewa orodha ya mbinu wakiombwa na watoataarifa kuchagua mbinu wanazotumia. Jedwali Na. 5.4 linaonesha mbinu zilizochaguliwa na watoataarifa.

**Jedwali Na. 5.4**: **Mbinu Zinazotumiwa na Walimu wa Kiswahili Kufundisha Vipengele vya Utamaduni**

| **Na.** | **Mbinu za Ufundishaji wa Utamaduni** | **Idadi ya Walimu** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|
| 1. | Majadiliano juu ya vitabu na matini za Kiswahili | 3 | 37.5 |
| 2. | Uchambuzi wa mashairi na hadithi | 2 | 25 |
| 3. | Usikilizaji wa nyimbo na mazungumzo ya wenyeji wa Kiswahili | 2 | 25 |
| 4. | Uigizaji | 4 | 50 |
| 5. | Majadiliano kuhusu ufanano na tofauti za kitamaduni | 2 | 25 |

**Chanzo:** Uwandani (2022-2023)

Jedwali Na. 5.4 linaonesha kuwa mbinu zinazothibitika kutumiwa na walimu katika kufundisha utamaduni wa Kiswahili ni pamoja na uigizaji unaotumiwa na walimu wanne miongoni mwa wanane, sawa na 50%, majadiliano juu ya vitabu na matini za Kiswahili yanayotumiwa na walimu wawatu, sawa na 37.5%. Mbinu za uchambuzi wa mashairi na hadithi, usikilizaji wa nyimbo na mazungumzo ya wenyeji wa Kiswahili na majadiliano kuhusu ufanano na tofauti za kitamaduni zilibainika kutumiwa na walimu wawiliwawili, sawa na 25%, kila moja**.**

Kutokana na matokeo hayo hapo juu, asilimia kubwa ya walimu (50%) hutumia mbinu ya uigizaji kwa kuwa inawapa wanafunzi fursa ya kukariri waliyoyasoma na kuyaweka katika vitendo. Jambo hilo linawahakikishia walimu ujuzi walioupata wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha na utamaduni wake. Pia, kwa mbinu ya majadiliano juu ya vitabu na matini za Kiswahili iliyosisitizwa na walimu watatu (37.5%), huwasaidia wanafunzi kuonesha uelewa wao kwa kutoa mawazo juu ya habari wanazozisoma darasani na kujenga misingi ya uandishi na uzungumzaji. Kuhusu matumizi ya mbinu ya uchambuzi wa mashairi na hadithi iliyothibitishwa kutumiwa na walimu kwa kiwango cha 25%, wale ambao hawakuitaja wameiona kuwa sehemu ya mbinu ya majadiliano juu ya vitabu na matini za Kiswahili. Hivyo, kwa mujibu wa walimu waliotoa taarifa, mbinu hiyo huwasaidia wanafunzi kujenga uwezo wa kimaandishi na kimazungumzo kwa kujipatia msamiati mpya na kujaribu kuutumia. Kuhusu mbinu ya usikilizaji wa nyimbo na mazungumzo ya wenyeji wa Kiswahili, walimu wanasema kuwa wana tatizo la kutopata kiurahisi vifaa vinavyoaminika. Hata hivyo, wanaoitumia mbinu hiyo wanaamini kuwa utamu wa nyimbo huwawezesha wanafunzi kukariri haraka dhana mpya na kuwapa motisha katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kuhusu mbinu ya majadiliano juu ya ufanano na tofauti za kitamaduni, walimu wawili, sawa na 25%, ndio waliokuwa wanashadidia matumizi yake, wengine wakihofia kutokuwa na ujuzi kamili juu ya utamaduni mwingine.

Kutokana na maelezo ya walimu hapo juu, ni dhahiri kuwa mbinu tajwa hapo juu na ambazo hutumiwa na walimu wa Kiswahili kwenye vyuo vikuu nchini Burundi ni mbinu shirikishi zinazoamsha ari ya wanafunzi kujifunza lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Hili linashadidiwa na Msigwa (2019) kuwa mbinu hizo zinawawezesha wanafunzi kuamili lugha na kuzipa nafasi katika maisha yao kwani huchangia katika kupata uelewa juu ya lugha na utamaduni unaoendana nayo.

## 5.5 Vifaa Vinavyotumiwa na Walimu wa Kiswahili katika Ufundishaji wa Utamaduni wa Kiswahili

Utafiti huu umechunguza pia vifaa vya kufundishia utamaduni wa Kiswahili. Hivyo, watoataarifa waliombwa kuchagua miongoni mwa vifaa vilivyotolewa na watafiti vile ambavyo wanavitumia katika ufundishaji wa utamaduni wa Kiswahili. Jedwali Na. 5.5 linaonesha vifaa vilivyoonekana kutumiwa na walimu tafitiwa.

**Jedwali Na. 5.5: Vifaa vya Kufundishia Utamaduni wa Kiswahili**

| Na. | Vifaa | Idadi ya Walimu | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 1. | Vitabu | 3 | 37.5 |
| 2. | Mashairi na hadithi ndogondogo | 2 | 25 |
| 3. | Redio | 2 | 25 |
| 4. | Intaneti | 3 | 37.5 |
| 5. | Video | 2 | 25 |
| 6. | Televisheni | 2 | 25 |
| 7. | Projekta | 4 | 50 |
| 8. | Kompyuta | 4 | 50 |

**Chanzo:** Uwandani (2022-2023)

Jedwali Na. 5.5 hapo juu linaonesha vifaa vya kufundishia utamaduni wa Kiswahili na idadi ya walimu waliothibitisha kuvitumia. Walimu wannewanne, sawa na 50% kila mara, ndio waliohakikisha kuwa wanatumia kompyuta na projekta katika ufundishaji wa utamaduni, ilhali watatuwatatu, sawa na 37.5% kila mara, ndio waliothibitika kutumia vitabu na intaneti. Mashairi na hadithi ndogondogo, video na televisheni navyo vilionekana kuwa vinatumiwa na walimu wawiliwawili kila mara, sawa na 25%.

Kwa mujibu wa walimu waliohusishwa katika utafiti, matumizi ya vifaa hivyo huwa yanachochewa na mahitaji kutokana na mbinu wanazozitumia. Kwa maneno mengine, walimu wamehakikisha kuwa mbinu wanazozitumia huwiana na vifaa tajwa hapo juu. Hivyo, katika ufundishaji kwa mijadala na matini, vitabu vinahitajika, ambapo ufundishaji kwa nyimbo umechochea matumizi ya redio na televisheni. Vilevile, kwa mujibu wa walimu, uhitaji wa kuwasilisha somo kiurahisi kwa wanafunzi ndio unaowalazimisha kutumia kompyuta, projekta na intaneti. Maoni hayo ya walimu yanawiana na matokeo ya watafiti kama Msigwa (2019) na Vicent na Msigwa (2021) wakizungumzia umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mchango wa media za video katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Kwa mujibu wao, vifaa kama hivyo ni shirikishi ambavyo huwawezesha wanafunzi kuamili lugha ya Kiswahili kwa kuwa huwaweka katika mazingira halisi.

## 6.0 Hitimisho

Utafiti huu ulichunguza mbinu zinazotumiwa na walimu wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Burundi katika ufundishaji wa utamaduni wa lugha husika. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba hakuna masomo kamili ya utamaduni katika mitaala ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Burundi bali vipengele vya utamaduni vinavyoingizwa na walimu kwenye baadhi ya masomo kwa utashi wao. Katika kufundisha masuala ya utamaduni yaliyobainika, kuna baadhi ya mbinu

zilizobainika kutumiwa na walimu kama vile majadiliano kuhusu vitabu na matini za Kiswahili, usomaji wa vitabu, uchambuzi wa mashairi na hadithi. Jambo hilo linawasaidia wanafunzi kuimarika na kunufaika katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Pia, inawarahisishia mawasiliano wakati wanapokutana na wazawa wa lugha hiyo ya Kiswahili. Kuhusu vifaa vya kufundishia utamaduni wa Kiswahili, vitabu na intaneti ndivyo vilivyobainika kutumiwa kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, utafiti huu unapendekeza walimu wapewe mafunzo ya kutosha kuhusu utamaduni wa Kiswahili. Aidha, walimu wafanye tafiti zaidi kwa ajili ya kupata mbinu nzuri za kufundishia ili kufanikisha ufundishaji wa utamaduni wa Kiswahili. Vilevile, walimu wapewe vifaa kama vile televisheni ili kufanikisha ufundishaji wa masuala ya utamaduni kwa kutazamia shughuli zinazohusiana na utamaduni wa Kiswahili kwa sababu wanafunzi wanapojifunza kwa kutazama, huelewa zaidi na huwa hawasahau. Mwisho, mitaala ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Burundi ifanyiwe maboresho ili kozi zinazohusika na utamaduni wa Kiswahili zipewe nafasi kwa sababu lugha na utamaduni haviwezi kutenganishwa.

## Marejeleo


Ali, S., Kazemian, B. na Mahar, I.H. (2015). "The Importance of Culture in Second and Foreign Language Learning." *Dinamika Ilmu*. 15(1): 2442-9651.

Ali, Y.N. (2017). Tathmini ya Utoaji wa Maelezo ya Utamaduni katika Kufundisha Kiswahili kama Lugha ya Kigeni. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Bamporubusa, M. (2012). Matatizo Yanayojitokeza katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili Sanifu katika Ngazi ya Pili ya Shule za Msingi Nchini Burundi. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Burundi.

Belkhir-Benmostefa, F.Z. (2017). The Impact of Culture Teaching to Enhance Learners' Interest and Competence in Foreign Language Learning and Communication: The Case of 1st Year EFL Students at Abou-Bekr Belkaid University. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Abou-Bekr.

Bennet, M.J., Bennet, M. na Allen, W. (2003). "Developing Intercultural Competence in the Language Classroom." Katika D. Lange na M. Paige (Wah.), *Culture as the Core Perspectives on Culture in Second Language Learning*. Greenwich, CT: Information Age Publishing. Kur. 237-270.

Bukuru, D. na Niyonkuru, L. (2016). *Historia Fupi ya Kiswahili Nchini Burundi na Changamoto za Kukiendeleza katika Sekta Mbalimbali za Kitaifa.* Dar es Salaam: BAKITA.

Butoyi, D. (2022). Makosa ya Kisarufi ya Wanafunzi wa Kingwana Wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Uchunguzi Kifani wa Vyuo Vikuu vya Burundi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Cakir, I. (2006). "Developing Cultural Awareness in Foreign Language Teaching. Online Submission." *Turkish Online Journal of Distance Education.* 7(3): 154-161.

Chimhundu, H. (1997). "Language Standardisation Without Policy or Planning: Zimbabwe as a Case Study." Katika U. Royneland (Mh.), *Language Contact and Language Conflict.* Harare: Volda College. Kur. 129-150.

CRELACS. (2023). *Stratégies pour un Aménagement Linguistique Cohérent au Burundi.* Bujumbura : Université du Burundi.

Emitt, M.P.J. na Komesaroff, L. (2003). *Language and Learning.* Oxford: Oxford University Press.

Gao, F. (2006). "Language is Culture-On Intercultural Communication". *Journal of Language and Linguistics*. 5(1): 58-67.

Idang, G.E. (2015). African Culture and Values. *Phronimon*. 16(2): 97-111.

IPA (2019). *Programme Actualisé de Baccalauréat de l'Institut de Pédagogie Appliquée*. Bujumbura: Université du Burundi.

King'ei, K. na Kobia, J. (2007). "Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya." *Nordic Journal of African Studies*. 16(3): 320-332.

Kumaravadivelu, B. (2008). *Cultural Globalization and Language Education*. London: Yale University Press.

Lantolf, J.P. (Mh.). (1994). "Sociocultural Theory and Second Language Learning: Introduction to the Special Issue." *The Modern Language Journal*. 78(4): 418-420.

Liyong, T. (1972). *The Popular Culture of East Africa*. Londres: Longman.

McKay, S. (2003). "Teaching English as an International Language: The Chilean context." *ELT Journal*. 57(2): 139-148.

Macaro, L. (2003). *Teaching and Learning a Second Language. A Review of Recent Research*. Oxford: Bookcraft Ltd.

Masebo, J.A. na Nyambari, C.M. (2016). *Nadharia ya Lugha, Kiswahili 1: Kidato cha 5 na*

*6.* Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha. Isimu na Nadharia. Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Moore, D. (2003). *Les Représentations des Langues et de Leur Apprentissage*. Paris: Didier.

Muaka, A., Nduwamahoro, A. na Butoyi, D. (2024). "Language Policy in Burundi." Katika E.M. Lisanza na L. Muaka (Wah.), *The Palgrave Handbook of Language Policies in Africa.* Springer Nature Switzerland AG. Kur. 140-159. https://doi.org/10.1007/978-3-031-57308-8_6.

Msigwa, A.B.G. (2019). “Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni.” *Mulika.* 38: 74-86.

Ndayisenga, C. (2022). Hali ya Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu Nchini Burundi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Ualimu Burundi (ENS).

Nduwamahoro, A. (2021). Evaluation du Programme de Formation d’Enseignants de Kiswahili à l’Université du Burundi. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha de Buea.

Samovar, L.A., Porter, R.E., McDaniel, E.R. na Roy, C.S. (2017). *Communication Between Cultures*. Toronto: Nelson Education.

Shreeb, M.A. (2009). “Culture in Foreign Language Teaching.” *Ahl Al-Bait Journal*. 1(7): 351-361.

Stern, F. (1992). *Failure of Illiberalism: Essays on Political Culture of Modern Germany*. New York: Columbia University Press.

Todd, L. (1981). *An Introduction to Linguistics.* London: Longman.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Lugha na Isimu.* Dar es Salaam: University Press.

UNODC. (2017). *Evaluation Handbook*. Vienna: United Nations.

Vicent, S. na Msigwa, A.B.G. (2019). “Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni.” *Mulika*. 40(2): 142-157.

Vygotsky, L.S. (1980). *Mind in Society.* Cambridge: Harvard University Press.

Wang, Y.A. na Kulich, S.J. (2014). “Intercultural Communication. Representation and Construction of Culture.” *Language and Intercultural Communication*. 14(4): 508-512.

Yule, G. (1993). *The Study of Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

Zou, H. (2012). “Language Identity and Cultural Difference.” *International Journal of Social Science and Humanity*. 2(6): 465-490.